# JUMUIYA ILIYOIDHINISHWA MUNGATA

# MAKUBALIANO YA UWEKEZAJI KWENYE KITALU CHA UWINDAJI LUNG'ONYA KWENYE ENEO LA HIFADHI YA WANYAMAPORI MUNGATA

UMETAYARISHWA CHINI YA KIFUNGU CHA 31(7) CHA SHERIA YA UHIFADHI WA WANYAMAPORI NA 5 YA MWAKA 2009

KATI YA

JUMUIYA ILIYOIDHINISHWA MUNGATA

NA

SUNSET TARANGIRE LIMITED

UMETAYARISHWA NA:
JUMUIYA ILIYOIDHINISHWA MUNGATA
S.L.P 28,
RUFIJI, PWANI
APRIL, 2022



SSA

NNM

Scanned with CamScanner

Makubaliano haya yanaingiwa leo tarehe...25......ya mwezi....Aprili.....mwaka 2022

**Baina ya**

**JUMUIYA ILIYOIDHINISHWA MUNGATA,** Jumuiya iliyoidhinishwa na kuanzishwa kisha kusajiliwa kwa madhumuni ya uhifadhi wa eneo la Hifadhi ya Wanyamapori NGARAMBE- TAPIKA na yenye anwani ya S.L.P 28, UTETE, RUFIJI –PWANI. Katika mkataba huu itajulikana kama Jumuiya iliyoidhinishwa ("Jumuiya iliyoidhinishwa") kwa upande mmoja;

**NA**

**SUNSET TARANGIRE LIMITED** kampuni ambayo imesajiliwa nchini kwa mujibu wa Sheria ya Usajili wa makampuni sura namba 212, kwa namba za usajili 138974146 na yenye anwani ya S.L.P 2150 ARUSHA TANZANIA ikijumuisha wakala wake. Katika mkataba huu itajulikana kama ("Mwekezaji") kwa upande mwingine,

**<u>AMBAPO</u>**

A. Jumuiya iliyoidhinishwa, kwaniaba ya wananchi wanaoishi kwenye eneo lililo chini ya mamlaka yake na kwa kuzingatia Katiba yake ina mamlaka ya kutoa eneo la uwekezaji la Kitalu cha Uwindaji Lung'onya kilichopo kwenye eneo la Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori MUNGATA katika wilaya ya Rufiji mkoa wa Pwani.

B. Mwekezaji ameomba kutoka Jumuiya iliyoidhinishwa kupewa kitalu cha uwindaji kwa ajili ya kuendesha biashara ya uwindaji wa kitalii.

C. Jumuiya iliyoidhinishwa imekubali na kumruhusu mwekezaji kuwekeza kwa kuzingatia vigezo na masharti yaliyoainishwa kwenye mkataba huu, sehemu ya eneo la Jumuiya iliyoidhinishwa lenye ukubwa wa kilomita za mraba 532.63 ambalo limetengwa kwa ajili ya shughuli za uwindaji wa kitalii. (hapa litajulikana kama "eneo").

D. Jumuiya iliyoidhinishwa na Mwekezaji wamekubaliana kuingia katika mkataba huu kwa lengo la Uwindaji wa kitalii, safari za kutazama wanyamapori na utalii wa picha (hapa yatajulikana kama **"makubaliano")**.



SSK

Mum

Scanned with CamScanner

**HIVYO, PANDE ZA MAKUBALIANO HAYA ZINAKUBALIANA KAMA IFUATAVYO:**

1. **MAANA NA TAFSIRI ZA MANENO**

Katika makubaliano haya isipokuwa pale itakapohitajika vinginevyo, maneno yafuatayo yatakuwa na maana kama ilivyooneshwa hapa chini:

a) ***"Tarehe ya kuanza"*** maana yake ni Tarehe ambayo makubaliano haya yamesaniwa na pande za zote mbili;

b) ***"Tarehe ya kuhitimisha"*** maana yake ni tarehe ya kuhitimisha uendelezaji wa mradi, au tarehe ya mwisho ya uwekezaji katika kitalu.

c) ***"Pango"*** maana yake ni makubaliano yakupangisha eneo pamoja na viambatishovyake na marekebishoyaliyoidhinishwa;

d) ***"Ada/kodi ya matumizi ya eneo"*** maana yake ni kodi, ada kwa mujibu wa ibara ya 7.1 ya makubaliano haya.

e) ***"Pande za makubaliano"*** maana yake ni Jumuiya iliyoidhinishwa na Mwekezaji, na matumizi ya umoja yatamanisha pande moja ya makubaliano;

f) ***"mipango na vipimo vya eneo"*** muonekana wa sakafu, sehemu, miinuko na alama au vipimo, na jedwali la muonekano wa mwisho utakaowasilishwa na msanifu majengo atakayekuwa ameajiriwa na mwekezaji kuhusu uendelezaji na kuambatanishwa kwenye makubaliano haya kama kiambatanisho B,

g) ***"Tarehe ya kuhitimisha sehemu ya undelezaji"*** maana yake ni tarehe ambapo sehemu ya uendelezaji imekamilika na kuthibitishwa kuwa imekamilika na meneja wa mradi;

h) ***"Mradi"*** maana yake itajumuisha utekelezaji na kuhitimishwa kwa uendelezaji;

i) ***"Huduma"*** inamaanisha miundombinu ya ndani ya eneo la uhifadhi kama vile barabara, mifumo ya utiririshaji maji, umeme, mifumo ya mawasiliano ya simu ndani ya eneo la uhifadhi, ambayo yatahusisha pande zote mbili za makubaliano hayahuu;

j) ***"Shughuli"*** itamanisha usanifu, ujenzi na taratibu za mifumo ya barabara ndaniya eneo la uendelezaji wa mradi, kusawazisha eneo kwa ajili ya ujenzi, uwekeaji wa huduma na ujenzi na ukamilishaji wa uendelezaji, yote kwa kuzingatia mipango na alama za vipimo.



SSA

Scanned with CamScanner

2. MASHARTI MAKUU YA MAKUBALIANO

2.1 Utekelezaji wa makubaliano haya utapaswa kuzingatia masharti makuu yafuatayo:

(a) Mipango sanifu na vipimo vya michoro kuidhinishwa kwa maandishi na Jumuiya iliyoidhinishwa, na idhini hiyo haitacheleweshwa wala kuzuiwa pasipo sababu za msingi;

(b) Mwekezaji kupata idhini kwa njia ya vibali vya maandishi kutoka serikalini na Halmasahuri au mamlaka za umma kwa ajili ya uendelezaji wa mradi kwa kuzingatia mipango sanifu na vipimo vya michoro. Kwa lengo hili Jumuiya iliyoidhinishwa itafanya kila linalowezekana kupata idhini husika.

3. MAJUKUMU YA PANDE ZA MAKUBALIANO HAYA

**3.1 Jumuiya Iliyoidhinishwa inakubali:**

i. Kuchukua hatua stahiki katika kutunza na kuendeleza eneo lote la Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori na kuhakikisha kwamba eneo halitumiki kwa makazi ya binadamu, yawe ya muda au ya kudumu au vinginevyo kwa kipindi chote cha makubaliano haya;

ii. Itamwezesha Mwekezaji na au mawakala wake katika kuingia kwenye eneo la Jumuiya wakati wote;

iii. Haitatoa haki ya matumizi kwa mtu au mwekezaji mwingine kuendesha biashara katika eneo ambalo linahusisha makubaliano haya na mwekazaji;

iv. Itatoa taarifa kwa mwekezaji kumhusisha katika mambo yote ambayo Jumuiya Iliyoidhinishwa inaamini kuwa yanaweza kuathiri uwekezaji na shughuli za uwekezaji ndani ya eneo la Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori;

v. Haitajiunga na jumuiya au kikundi kingine bila kumjusha mwekezaji kwa maandishi;



SSR

MNM

vi. Itaitisha mikutano yake ya kawaida ya kiutendaji kwa kuzingatia makubaliano kama itakavyokubaliwa kati ya mwekezaji na Jumuiya Iliyoidhinishwa.

**3.2 Mwekezaji anakubali kwamba:**

i. Kutoa fedha zote zitakazo hitajika kwa ajili ya kufanikisha uwekezaji;

ii. Kutoa vifaa na mali zingine zitakazohitajika kwa ajili ya kufanikisha uwekezaji;

iii. Kwamba mali zote zisizo hamishika na za kudumu ambazo kuondolewa kwake kunaweza kusababisha uharibifu wa mazingira zitakuwa mali ya Jumuiya Iliyoidhinishwa baada ya kuhitimishwa kwa makubaliano haya.

iv. Kujenga na kutunza miundo mbinu muhimu ya majengo;

v. Kutambua na kuziheshimu mila na desturi za wananchi wakaazi wa eneo hilo;

vi. Kutangaza eneo la Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori;

vii. Kuiepusha Jumuiya iliyoidhinishwa na athari za kiuchumi au madeni yanayoweza kujitokeza kutokana na makubaliano haya;

viii. Kutoa mafunzo na kuajiri wananchi wakaazi katika shughuli za kila siku za uwekezaji. Kimsingi, mwekezaji atajitahidi kuajiri angalau 60% ya wafanyakazi wake kutoka katika vijiji vinavyounda Jumuiya iliyoidhinishwa.

ix. Kupanga, kutekeleza na kuendeleza miradi mbalimbali yenye manufaa katika jamii;

x. Kuwajengea wananchi miundombinu ya msingi na mahitaji kwa mujibu wa makubaliano na Jumuiya iliyoidhinishwa;

xi. Kuwaruhusu wananchi kufanya shughuli za kiutamaduni kwa sharti kwamba shughuli hizo haziathiri miundombinu na shughuli za uwekezaji;

xii. Kuhakikisha kwamba uwekezaji umefanyiwa tathimini ya athari za mazingira kabla ya kuanza na shughuli za uendeshaji zitazingatia kanuni na miongozo iliyopo ya athari za mazingira;



SSA

mam

xiii. Hataingilia au kukwamisha au kutumia kwa maslahi ya kisiasa, kifedha au kiuchumi au kwa namna nyingine yoyote kwa nia ya kushawishi utendaji wa shughuli za kila siku za Jumuiya Iliyoidhinishwa kwa manufaa yake;

xiv. Hataingiza au kuruhusu uwepo wa mifugo au wanyama wafugwao nyumbani;

xv. Haitatumia ardhi iliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji kwa lengo lingine lolote, isipokuwa kwa malengo yaliyoombwa na kuidhinishwa kwa mujibu wa makubaliano haya, isipokuwa kwa idhini ya maandishi ya Jumuiya iliyoidhinishwa.

xvi. Hatapangisha au kuhamisha kwa namna yoyote ile makubaliano haya au sehemu ya makubaliano haya bila idhini ya maandishi ya Jumuiya iliyoidhinishwa ambayo itapatikana kwenye mkutano mkuu wa Jumuiya Iliyoidhinishwa utakaoitishwa kwa lengo la kujadili ombi hilo.

*xvii.* Kwamba eneo lote lenye mali zote zinazohamishika na zisizohamishika lililotumika kwenye uwekezaji litakuwa eneo la mwekezaji na kwamba mwekezaji hatakopa, kukodi, kupangisha mali yoyote isiyohamishika kwa lengo la kutumia vifaa hivyo bila idhini ya Jumuiya Iliyoidhinishwa.

*xviii.* Atapeleka askari wa wanyamapori wa vijiji walioajiriwa na jumuiya iliyoidhinishwa wawili (2) kila mwaka kwenda kupata mafunzo ya uhifadhi wa wanyamapori kwenye chuo cha uhifadhi wa wanyamapori kinachotambulika na Serikali

*xix.* Itatoa sare za maaskari mbili kila miaka mitano ya uwekezaji.

*xx.* Itajenga madarasa mawili kila mwaka katika shule itakayopendekezwa na jumuiya iliyoidhinishwa.

*xxi.* Itachimba kisima kimoja kirefu kila mwaka kwa mujibu wa maelekezo ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya Rufiji.

*xxii.* Itafungua barabara zote korofi za vijiji vya Ng'arambe na Tapika.

*xxiii.* Itachimba mabwawa manne ndani ya eneo la mawindo kwa kipindi cha miaka mitano tangu kuanza kwa mkataba.

*xxiv.* Itawakatia bima za afya wazee mia moja (100) waliomo ndani ya Jumuiya ya MUNGATA kila mwaka.



SSR

Mnm

*xxv.* Itapiga mkuza (alama za mipaka) ya eneo lote la jumuiya iliyoidhinishwa.

*xxvi.* Itakabidhi gari kwa jumuiya yenye thamani ya Tshs 70,000,000/= kwa ajili ya shughuli za doria. Umiliki wa gari hilo utakuwa chini ya Jumuiya iliyoidhinishwa (MUNGATA).

*xxvii.* Itakabidhi piki piki mpya sita (6) kwa jumuiya iliyoidhinishwa kwa ajili ya doria za kitalu hicho na shughuli nyinginezo. Umiliki wa pikipiki hizo utakuwa chini ya Jumuiya iliyoidhinishwa.

4. USIMAMIZI WA RASILIMALI

Mwekezaji anakubali kufanya yafuatayo:

i. Kufanya kila linalowezekana katika kuzuia mmomonyoko wa udongo na aina nyingine yoyote ya uharibifu wa mazingira kwenye eneo la jumuiya ya hifadhi wanyamapori.

ii. Kutoondoa, kuuza, kuharibu au kuhamisha kwa njia nyingine yoyote mchanga, kaburi, mawe, au mbao isipokuwa kwa kuzingatia sheria.

iii. Kwamba hataharibu au kukata miti kwa njia yoyote ile isipokuwa kwa idhini ya Jumuiya iliyoidhinishwa.

5. KUHAMISHA HAKI ZA UMILIKI

Mwekezaji anakubali kutopangisha, au kuhamisha haki yake ya umiliki au kuachana na usimamizi wa eneo la uwekezaji au sehemu yake iliyotolewa kwa lengo la uwekezaji na Jumuiya iliyoidhinishwa.

6. DHAMANA YA UTEKELEZAJI

Mwekezaji atatoa fedha ya dhamana ya utekelezaji ya Dola elfu thelathini za kimarekani (**USD 30,000**) ambazo zitawekwa katika akaunti ya pamoja ya Mwekezaji na Jumuiya iliyoidhinishwa kama dhamana ya kuendeleza uwekezaji. Kiasi hicho cha fedha pamoja na riba itakayotokana na kiasi hicho zitachukuliwa na Jumuiya iliyoidhinishwa pale ambapo Mwekezaji ama, atatoroka au kutelekeza mradi huo wa uwekezaji au zitakapohitajika kwa ajili ya kukaza hukumu dhidi ya mwekezaji pale ambapo Mwekezaji ameshindwa kulipa malipo



SSA

MNM

Scanned with CamScanner

yanayotakiwa. Vinginevyo, Fedha hiyo ya dhamana ya utekelezaji pamoja na riba yake itarejeshwa kwa Mwekezaji mwisho wa mkataba ukifika.

## 7. ADA KWA AJILI YA HAKI YA KUENDESHA SHUGHULI.

Kwamba ada kwa ajili ya kuendesha shughuli za uwekezaji zitatozwa kwa kuzingatia viwango vifuatavyo:

(1) Mwekezaji atalipa kiasi cha dola elfu thelathini **(USD 30,000)** za kimarekani kila mwaka kama ada ya kitalu na dola elfu moja **(USD 1,000)** ikiwa ni nyiongeza ya ada ya kitalu kwa mwaka kwa ajili ya shughuli za uwindaji wa kitalii kwa Jumuiya iliyoidhinishwa kwenye kitalu cha Lung'onya chenye ukubwa wa kilometa za mraba 532.63 Eneo ambalo limetengwa kama Kitalu cha uwindaji wa kitalii.

(2) Ada ya kitalu cha uwindaji kwa ajili ya shughuli za uwindaji wa kitalii kama ilivyoainishwa kwenye ibara ya 7.1 ya makubaliano haya kwa mwaka wa kwanza italipwa mara tu baada ya kusainiwa kwa makubaliano haya na kwa miaka mingine yote iliyobaki ada hii italipwa kila mwezi Machi kwa mwaka husika.

(3) Mwekezaji atalipa dola za kimarekani elfu kumi **(USD 10,000)** kila mwaka kama mchango wa maendeleo ya jamii kwenye vijiji vinavyounda jumuiya.

(4) Mwekezaji atalipa kiasi cha dola za kimarekani elfu kumi **(USD 10,000)** kwa Jumuiya ikiwa ni mchango wa gharama za kudhibiti ujangili kwenye eneo la Jumuiya iliyoidhinishwa kila mwaka.

## 8. MAMBO YASIYOWEZA KUZUILIWA NA PANDE MBILI ZA MAKUBALIANO HAYA.

(1) Endapo litatokea jambo lolote lililo nje ya uwezo wa kuzuiwa na pande mbili za makubaliano haya, na hivyo kufanya upande mmoja au pande zote mbili kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa makubaliano haya kwa kiwango kile atakachokuwa ameshindwa kutekeleza na haiwezekani kwa upande ulioathirika kuweza kulipwa kikamilifu na bima, na kwamba kushindwa huko hakutaufanya upande mmoja kuwajibika kwa upande mwingine.



GSA

Mdm

(2) Endapo jambo lolote lililo nje ya uwezo wa kuzuiliwa na pande mbili za makubaliano haya litaendelea kwa miezi mitatu au zaidi na jambo hilo linauzuia upande mmoja wa makubaliano kwa ujumla au kwa sehemu kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa makubaliano haya basi upande ule ambao umeshindwa kutekeleza majukumu yake unaweza, kwa maandishi kupeleka notisi upande mwingine kusitisha haki zote na majukumu yanayotokana na makubaliano haya kwa jinsi itakavyokuwa hadi pale jambo hilo lililo nje ya uwezo wa kuzuiliwa na pande mbili za makubaliano haya litakapokoma na pande mbili za makubaliano haya wanaweza kuanza kutekeleza majukumu yao husika:

Ikizingatiwa kwamba, kama notisi hiyo itatolewa na mwekezaji ataruhusiwa kuingia katika Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori kuchukua hatua za kulinda mali zake katika kipindi cha usitishwaji. Pande za makubaliano haya zitaanza kutekeleza majukumu yao kwa notisi ya maandishi itakayotolewa na upande ulioathirika.

(3) Kwa mujibu wa makubaliano haya '**jambo lisiloweza kuzuiwa na pande za makubaliano** lina maana ya jambo lolote kati ya haya yafuatayo ambalo laweza kwa kiasi kikubwa kuathiri biashara, loji, mmiliki au uwezo wa mwekezaji kushiriki katika ujenzi na usimamizi wa loji: jambo linatokana na uwezo wa Mungu (ikiwa ni pamoja na haitaishia kwa tetemeko la ardhi, mafuriko au mlipuko wa volkano), magonjwa ya mlipuko au hali nyingine yoyote inayopunguza au kuondoa kabisa uwezo wa kawaida wa binadamu kimwili au viumbe vingine na ambayo yanaambukizwa kwa binadamu, kutekeleza majukumu yake au kuathiri viumbe wengine yanayoweza kusababishwa na vita, ugaidi, machafuko, migomo, kufungwa kwa maeneo ya kazi au mgogoro mwingine wowote kuhusiana na ajira, moto, mafuriko, sheria za nchi, vikwazo vya kiuchumi, vita vya wenyewe kwa wenyewe, vikwazo vya kibiashara au sababu yoyote ya kiuchumi mbayo ni vigumu kukabiliana nayo katika hali ya kawaida kwa upande wowote wa makubaliano haya, lakini hii haitahusisha tukio lolote lile ambalo litasababishwa na upande wowote wa makubaliano haya.

SSA



M.N.M.

9. HAKI YA UMILIKI

9.1 Bila kuathiri kuanza kwa utekelezwaji wa makubaliano haya, Mwekezaji atakuwa na haki ya kumiliki kuanzia tarehe…………… mwezi………… mwaka………… Jumuiya iliyoidhinishwa ikithibitisha kwamba hakutakuwa na kizuizi chochote kwa mwekezaji katika kumiliki au kutwaa ardhi.

9.2 Madhara yatokanayo na kumiliki eneo kabla ya kuanza kutekelezwa kwa masharti muhimu yatabebwa na mwekezaji na atawajibika endapo masharti hayo hayakutekelezwa kuhakikisha anaondoka mara moja kwenye eneo na kulirudisha eneo kwa Jumuiya iliyoidhinishwa katika hali ya awali baada ya kupokea notisi ya kuondoka itakayotolewa na Jumuiya iliyoidhinishwa.

9.3 Kwa kuziangatia masharti yaliyowekwa, na kama umiliki kamili haujafanyika kwa kipindi hicho, mwekezaji atachukuliwa kuwa amemiliki eneo katika tarehe ambapo masharti yaliyoainishwa kwenye aya ya 2.0 yatakuwa yametimizwa.

10. PANGO

10.1 Kwa kuzingatia masharti na vigezo vilivyoianishwa, Jumuiya iliyidhinishwa inapangisha eneo kwa mwekezaji ambaye hapa anapanga eneo hilo.

10.2 Upande wowote wa makubaliano haya hautaruhusiwa kubadili matumizi ya eneo na kwa makubaliano haya mwekezaji anakubali kutumia eneo kwa mujibu wa sheria na kufuata sheria na sheria ndogo.

11. UENDESHAJI NA MUDA WA UTEKELEZAJI

11.1 Kwa kuzingatia matakwa ya makubaliano haya na bila kuathiri sheria nyingine, ambazo makubaliano haya yanazifuata, makubaliano haya yatakuchukuliwa kuwa yanaanza rasmi tarehe ambayo yatasainiwa na watu wenye mamlaka kwa niaba ya pande mbili za makubaliano ambao wamepewa mamalaka ya kufanya hivyo. Makubaliano haya yatatekelezwa kwa kipindi cha miaka kumi (10) kwamba makubaliano haya yanaweza kuhuishwa. Endapo mwekezaji hata vunja masharti ya Makubaliano, makubaliano haya yanaweza kuhuishwa tena kwa kipindi cha miaka kumi (10) kwa kuzingatia kwamba mwekezaji atatoa notisi ya mwaka mmoja kwa Jumuiya iliyoidhinishwa na notisi ya

SSR



M.N.M

Scanned with CamScanner

kukumbushia miezi sita baada ya kutolewa kwa notisi ya kwanza kabla ya kuisha kwa kipindi cha makubaliano haya.

11.2 Iwapo mwekezaji hatakuwa na nia ya kuendelea na uendeshaji wa eneo husika baada ya kukoma kwa makubaliano, mwekezaji hatakuwa na haki ya kuhamisha haki alizopata chini ya makubaliano haya na mali zote zisizohamishika zitakuwa mali za jumuiyai liyoidhinishwa.

12. KUVUNJIKA KWA MAKUBALIANO

12.1 Makubaliano haya yatasitishwa moja kwa moja pale ambapo Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori ataondoa au kufuta haki ya Matumizi ya Rasilimali ya Wanyamapori iliyotolewa kwa Jumuiya;

12.2 Upande wowote wa makubaliano una haki ya kusitisha makubaliano haya endapo upande mwingine wa makubaliano utakuwa umefanya ukiukwaji/uvunjaji mkubwa wa masharti ya makubaliano;

12.3 Uvunjaji Mkubwa wa Makubaliano utajumuisha yafuatayo:

(a) Mwekezaji akishindwa kutekeleza au kufuata jukumu au wajibu wowote aliopewa chini ya makubaliano haya, na kama akishindwa kurekebisha uvunjaji huo ndani ya siku 60 baada ya kupewa taarifa (notisi) na Jumuiya Iliyoidhinishwa ikimtaka kurekebisha uvunjaji huo;

(b) Ikiwa Mwekezaji atafilisika au kampuni itafungwa kisheria isipokuwa kama Mwekezaji atakuwa anaundwa upya kisheria au kuunganishwa;

(c) Ikiwa Mwekezaji atacheleweshwa kumalizika kwa uwekezaji kwa mujibu wa makubaliano baada ya muda wa kuanza uwekezaji au muda mwingine watakaokuwa wamekubaliana kwa maandishi;

(d) Bila kujali haya yote, Jumuiya Iliyoidhinishwa, inaweza kusitisha Makubaliano haya kwa kuzingatia manufaa yake.

i. Iwapo Makubaliano yatasitishwa, Mwekezaji atatakiwa kusimamisha shughuli zake mara moja, na kulifanya eneo la uwekezaji kuwa salama na ataondoka katika eneo husika mapema iwezekanavyo.

SSP



MNM

Scanned with CamScanner

12.4 Kama Makubaliano yatasitishwa kwa kuzingatia manufaa ya Jumuiya iliyoidhinishwa au kutokana na uvunjaji mkubwa wa Mkataba kwa Jumuiya; wahusika wataweka Mthamini huru atakayetoa hati ya thamani ya gharama za Mwekezaji katika eneo ambapo Mwekezaji atatakiwa kufidiwa.

13. **DHAMANA/REHANI**

13.1 Iwapo gharama za uendelezaji wa uwekezaji unahitaji kuweka rehani itakayosajiliwa kwa mujibu wa eneo, Jumuiya iliyoidhinishwa itatakiwa kutoa idhini; ikizingatiwa kwamba rehani hiyo itakuwa ni kwa lengo la uwekezaji husika, itakuwa kwa lengo la kuweka rehani maslahi ya mwekezaji kwenye upangishaji kwa muda wa upangaji uliobakia na haitakuwa na athari ya umiliki wa eneo husika kwa Jumuiya iliyoidhinishwa.

14. **NOTISI**

14.1 Pande zote za makubaliano, zinachagua, kwa ajili ya kutoa notisi, kutoa malipo ya kiasi chochote, na kwa lengo lingine lolote, litakalotokana na makubaliano haya, itawasilishwa kwenye anwani zao husika kama ifuatavyo:

(a) Mwenyekiti,
Jumuiya iliyoidhinishwa ya Mungata.
S.L.P. 28,
UTETE, RUFIJI
TANZANIA.

(b) Mkurugenzi,
Sunset Tarangire Safaris Limited,
S.L.P 2150
Arusha, Tanzania.

14.2 Upande wowote unaweza kubadili anwani ndani ya Tanzania kwa kutoa taarifa ya maandishi ndani ya siku kumi na nne (14) au Mbia anaweza pia kubadili



SSF

Mnm

Scanned with CamScanner

anwani yake katika nchi yake ya asili kwa kutoa taarifa au notisi ya siku kumi na nne (14).

14.3 Notisi yoyote itakayotolewa au malipo yatakayofanywa na upande wowote kwa upande mwingine ("mpokeaji") yatakuwa kamilifu kwa upande unaotumiwa endapo:

(a) Yakipelekwa kwa mkono au kwa njia ya barua pepe muda wa kawaida wa saa za kazi, yatachukuliwa kuwa yamepokelewa na mpokeaji siku inayofuata baada ya kuwasilishwa au siku ya kuwasilisha barua pepe;

(b) Yatatumwa kwa njia ya posta kutoka katika anwani ya nchi ya asili ya Mwekezaji au nchini Tanzania itachukuliwa kuwa yamepokelewa na mpokeaji siku ya tano ya siku za kazi baada ya kutumwa.

14.4 Endapo upande wowote wa makubaliano haya umeomba idhini kwa maandishi chini ya ibara yeyote ya makubaliano haya, itachukuliwa kwamba idhini hiyo imetolewa endapo aliyeombwa idhini hiyo hatajibu ndani ya siku ishirini na moja (21) baada ya maombi ya idhini hiyo kufika katika anwani zilizoainishwa katika ibara ya 14.1.

15. UTATUZI WA MIGOGORO

15.1 Endapo mgogoro utatokea kutokana na makubaliano haya, upande wowote wa makubaliano haya utakuwa na haki ya kuujulisha upande mwingine kwa notisi ya maandishi kuwa mgogoro upelekwe kwa uamuzi kwa mujibu wa Ibaraya 15. Ili kuondoa mashaka, ibaraya 15 itatumika kwa migogoro yote itakayotokea.

15.2 Baada ya kupokea notisi ya maandishi iliyotajwa kwenye ibara ya 15.1 pande mbili za makubaliano zitakutana ili kuutatua mgogoro kwa nia njema kwa haraka iwezekanavyo.

15.3 Endapo pande za makubaliano zitashindwa kuutatua mgogoro pamoja na kuzingatia ibara ya 15.2 basi mgogoro huo utapalekwa kwa mwamuzi hasa waamuzi watatu kwa mujibu wa matakwa ya kanuni zingine za Ibara ya 15.



GSK

MNM

Scanned with CamScanner

15.4 Kwa kuzingatia ibara zilizotangulia za ibara ya 15 na kwa kuzingatia jambo linalopaswa kutolewa uamuzi mwamuzi/waamuzi watakuwa:

a) Endapo ni kwa jambo linalohusisha fedha, mbia mfawidhi kwa wakati huo mwenye uzoefu wa kimataifa katika usimamizi wa fedha ambaye ni mkazi wa Arusha.
b) Endapo ni kwa mambo ya kisheria, wakili mwandamizi kutoka chama cha mawakili, jaji mstaafu au mwanasheria mkuu wa serikali.
c) Kwa jambo lingine lolote, mtu mwenye sifa husika na uzoefu kama itakavyokubaliwa na pande mbili kwa maandishi au kwa kusajili makubaliano ndani ya siku 14, atateuliwa na Rais wa wakati huo wa Mahakama ya Afrika Mashariki iliyopo Arusha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye ataombwa na upande wowote kufanya uteuzi wakati wowote baada ya kumalizika kwa siku 14.

15.5 Uamuzi utazingatia sheria za Jamhuriya Muungano wa Tanzania

15.6 Waamuzi watakuwa na haki ya:

a) Kuomba na kukagua nyaraka au kumbukumbu ambazo zinahusu suala linalobishaniwa na kutoa nakala na anaweza kuomba zitolewe nakala na anaweza kuomba zitolewe na kuwasilishwa mahali popote atakapoona zinahitajika kwa kazi hiyo husika.
b) Kufanya mahojiano na maswali kwa wawakilishi na mashahidi wa upande wowote chini ya kiapo.
c) Kutoa tuzo ya uamuzi kwa ajili ya kumtaka aliyekiuka makubaliano haya kutekeleza majukumu yake, zuio, vitulizo vya mahakama au adhabu au kwa kadri atakavyoona inafaa.

15.7 Uamuzi utafanyika mapema iwezekanavyo lengo likiwa ni kuhakikisha kuwa uamuzi huo unakamilika ndani ya siku sitini (60) baada ya kuteuliwa kwa waamuzi.

15.8 Mara baada ya waamuzi kukubaliwa na pande zote mbili au kuteuliwa kwa mujibu wa ibara ya 15.4 upande wowote utakuwa na haki ya kuwaomba waamuzi kupanga tarehe na mahali ambapo mashauri ya uamuzi yatafanyika. Mashauri ya uamuzi yatafanyika kwa siri na pande husika zitahakikisha kuwa zinatunza siri.



SSK

MNM

Scanned with CamScanner

15.9 Tuzo yeyote itakayotolewa na waamuzi:

a) Itakuwa kwa maandishi ikieleza sababu za uamuzi husika;
b) Itakuwa ndio uamuazi wa mwisho na unao zifunga pande za makubaliano
c) itatekelezwa;

15.10 Endapo makubaliano haya yatasitishwa kwa sababu yeyote ile, masharti ya ibara ya 15 yataendelea kutumika baada ya usitishwaji huo.

15.11 Kwa kuzingatia ibara ya 15(12), makubaliano ya Ibara ya 15 yatachukuliwa kuwa ni ridhaa isiyoweza kusitishwa na pande za makubaliano haya kwa mashauri yote na kwamba hakuna upande utakaokuwa na haki ya kujiondoa au kuomba katika mashauri yeyote kwamba haufungwi na ibara ya 15.

15.12 Ibara ya 15 haitatumika kuuondoa upande wowote kwa njia ya kufungua mashauri kwa jambo la dharura kwenye mahakama wakati ukisubiriwa uamuzi wa muamuzi,

16. <u>MAELEZO YA JUMLA NA HITIMISHO</u>

16.1 Makubaliano haya na viambatanishi vyote vya mkataba huu kwa pamoja vinakamilisha makubaliano baina ya pande mbili za makubaliano haya na kwamba hakuna mabadiliko au kuondolewa kwa kifungu chochote ambako kutakuwa sahihi isipokuwa tu endapo mabadiliko hayo yatafanyika kwa maandishi na kusainiwa na wawakilishi wenye mamlaka ya kusaini kwa niaba ya pande husika, na kwamba hakuatakuwa na aina yoyote ya utekelezaji au kutaka kutekezwa ambayo itachukuliwa kuwa sehemu ya makubaliano haya isipokuwa kwa yale tu yaliyomo katika makubaliano haya.

16.2 Kuridhia kwa aina yoyote ya kuvunjwa kwa kipengele chochote cha makubaliano haya na upande wowote hayatachukuliwa kama kusamehe kwa upande wowote na hivyo kuondoa haki kwa upande ambao haukutendewa haki kuhusiana na makubaliano haya kudai hakiyake.

16.3 Makubaliano haya yatachukuliwa na kutafsiriwa kwa kuzingatia sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

SSA



NM

Scanned with CamScanner

16.4 Kwamba pande zote mbili zinakubaliana kwa pamoja kuhakikisha kwamba zinatekeleza kikamilifu na kutoa msaada wowote utakaohitajika ili kuhakikisha kuwa makubaliano haya yanatekelezwa kikamilifu.

16.5 Endapo kutakuwa na ruhusa au ombi la kufanya jambo lolote ambalo haliathiri makubaliano haya basi ruhusa hiyo haitazuiliwa au kucheleweshwa bila sababu za msingi.

16.6 Gharama zote kuhusiana na mapatano, maandalizi, utekelezaji na usajili wa makubaliano haya, na kukutana kwa pande husika kuhusiana na makubaliano haya zitagharamiwa na mwekezaji.



SSA

h N m

**SAINI**

Imeshuhudiwa, kutiwa Mhuri na kukabidhiwa na Jumuiya ya Uhifadhi wa Wanyamapori Mungata; na Mwekezaji na kwamba wameridhia makubaliano haya kwa tarehe zilizo tajwa hapa chini.

Kwa niaba ya ***Jumuiya ya Hifadhi wa Wanyamapori MUNGATA;***

...................................

(saini)

Jina: MWAJUMA -N. MKWINDI

(Jina la afisa aliyeruhusiwa kusaini)

JUMUIYA YA KUHIFADHI MALIASILI (MUNGATA) S.L.P. 28 UTETE - RUFIJI

UTETE/RUFIJI

(Mahali/Mji)

MHURI

Leo 25 siku ya APR 2022

Wadhifa: MWENYEKITI WA BODI YA WADHAMINI MUNGATA

Kwa niaba ya ***Sunset Tarangire limited;***

...................................

(saini)

Jina: SALEH SALIM AL-MRY

(Jina la afisa aliyeruhusiwa kusaini)

SUNSET TARANGIRE LIMITED P.O. Box 15128 ARUSHA

UTETE - RUFIJI

(Mahali/Mji)

MHURI

Leo 25 siku ya APRIL 2022

Wadhifa: MKURUGENZI MKUU

SSA



MNM

Scanned with CamScanner

**Mbele ya:**

Jina: LEAH KIMARO

Saini: ...................

Wadhifa: MWANASHERIA (W) RUFIJI

Tarehe: 25/04/2022

MWANASHERIA
S.L.P 28
UTETE-RUFIJI
HALMASHAURI YA WILAYA RUFIJI



SSA

MNM